

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



Barabara ya Nyerere  
S.L.P 377 Musoma  
Simu: 028-2623029 Nukushi: 028- 2623030  
Barua pepe: [rbcmara@pccb.go.tz](mailto:rbcmara@pccb.go.tz)  
Wavuti [www.pccb.go.tz](http://www.pccb.go.tz)

---

---

**TAARIFA KWA UMMA**

---

---

**TAARIFA YA UTENDAJI KAZI TAKUKURU MKOA WA MARA**  
**KIPINDI CHA JULAI –SEPTEMBER 2020**

**Ndugu wana Habari,**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Mara katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita yaani Julai hadi Septemba 2020, ilikuwa na mambo makubwa manne iliyoyafanya.

**Kwanza,**

Ni kufuatilia kwa karibu zoezi la kampeni ili kuhakikisha kuwa vitendo vya rushwa havipati nafasi wakati wa kampeni za kuwania nafasi mbalimbali za kisiasa.

Katika kipindi hiki cha kampeni tulipokea jumla ya tuhuma 51 zikiwahusu wagombea mbalimbali pamoja na wafuasi wao kujihusisha na vitendo vya rushwa. Kati ya tuhuma hizo, tuhuma 33 sawa na asilimia 65% ziliwasilishwa na wanafunzi wa shule za sekondari ambao ni wanachama wa Klabu za Wapinga Rushwa.

## **Pili,**

Tuliendelea na zoezi letu la kuwapigania wastaafu dhidi ya mikopo umiza ambapo katika kipindi hiki cha miezi mitatu tuliwasaidia jumla ya wastaafu watano na kufanikiwa kuwarejeshea fedha - kiasi cha Tsh

**235,905,000/=** ambapo kiasi cha Tsh **18,705,000/=** sawa na **7.3%** zilirudishwa Serikalini na **92.7%** ya fedha zote zilizookolewa zilirejeshwa mikononi mwa wananchi wanyonge waliokuwa wamedhulumwa.

## **Tatu,**

Katika upande wa Waendesha Mastaka - jumla ya kesi 11 zilitolewa maamuzi ambapo kesi 9 sawa 81.8% watuhumiwa walitiwa hatiani kwa adhabu tofauti ambapo katika kesi hizo watuhumiwa wanne walitakiwa kulipa TAKUKURU jumla ya Tsh 10,500,000/= na wote wakitiwa hatiani kwa kwenda jela miaka miamatu au kulipa faini ya Tsh500,000/=.

Moja kati ya kesi hizi ni ile iliyo mhusu Mheshimiwa Hakim aliyekuwa akiwasaidia wakopeshaji wa Mikopo umiza ili kuwadhulumu wastaafu. Yeye alihukumiwa kwenda jela mika mitatu au kulipa faini ya Tsh 500,000/=.

## **Nne,**

Katika eneo la uchunguzi TAKUKURU mkoa wa Mara ilinusa uwepo wa ufiadi mkubwa katika ufunguaji na usimamizi wa mirathi ambapo jumla ya watuhumiwa wanne katika tuhuma mbili tofauti wanachunguzwa.

Katika tuhuma hizi watuhumiwa wanadaiwa kujinufaisha kwa kujipatia jumla ya Tsh **112.3 bilioni** kwa kipindi cha miaka 21 kwa mirathi hewa waliyoifungua Mahakamani.

Vile vile, kwa kipindi chote hicho wajane na watoto wa marehemu wamekuwa wakiishi maisha ya shida sana hata kufikia kushindwa kuwasomesha watoto wa marehemu katika shule nzuri huku watuhumiwa hao wakiendelea kuishi maisha mazuri kwa jasho la marehemu.

Uchunguzi dhidi ya tuhuma hii unaendelea na punde tutakapokamilisha uchunguzi wetu watuhumiwa watafikishwa katika vyombo vya sheria kujibu tuhuma zinazo wakabili.

**ALEX J KUHANDA  
MKUU WA TAKUKURU  
MKOA WA MARA**